Tufuatilie kupitia Kilosa DC www.kilosadc.go.tz 0737847749

# Kilosa Yetu

*Fungua Fikra*

Halmashauri ya Wilaya yaKilosa: Toleo Na. 0004:Jarida Maalum la Ziara ya Rais

# ZIARA YA RAIS SAMIA WILAYANI KILOSA



## NDANI


- Uzinduzi wa Miradi
- Hotuba za Wabunge
- Salamu za Rais kwa Wananchi wa Kilosa
- Kauli za Mawaziri Mbalimbali


Imetolewa na Halmashauri ya Kilosa, Kitengo cha Mawasiliano Serikalini; www.kilosadc.go.tz

# Uzinduzi wa Daraja la Berega

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akizindua Rasmi Daraja la Berega lenye urefu wa mita 150 na upana wa mita 10 ambalo ujenzi wake umegharimu zaidi ya shilingi bilioni 7.9. Kukamilika kwa daraja hili kumerahisisha usafiri na usafirishaji kwa wakazi wa wilaya ya Kilosa na maeneo jirani.




Akiongea na wananchi wa Berega, Mhe. Rais amewataka wananchi ambao ni wanufaika wa daraja hilo kulitunza ikiwa ni pamoja na kutofanya shughuli za kiuchumi kama vile uchimbaji wa mchanga karibu na kingo za mto huo ili kuepusha uharibifu wa daraja hilo.

Aidha Rais Samia amesema daraja hilo litasaidia kuinua uchumi wa wananchi wa Mkoa wa Morogoro na Tanga.

> "*... najua watu wa Kilosa ni wakulima... Daraja hili litasaidia kusafirisha mazao yenu*







# Rais Samia Afungua Barabara Rudewa - Kilosa Urefu Km 24






Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amezindua barabara ya Rudewa - Kilosa yenye urefu wa kilometa 24 ikiwa mradi huu umegharimu shilingi bilioni 45.6.

Akizindua mradi huo, Rais Samia amesema kuwa mradi huu wa barabara utarahisisha shughuli za usafirishaji wa wananchi na bidhaa zao hivyo kushamiri kwa biashara na kupandisha uchumi wa Kilosa.

Katika hatua nyingine, Mhe. Rais ameipongeza TANRONDS na wakandarasi wazawa kwa kukamilisha mradi huo wa barabara amabao utaleta tija kwa wananchi na kuwataka wananchi kuitunza miundombinu yote iliyotekelezwa wailayani hapo.

RADIO JAMII KILOSA
Tunasikika kupitia 102.5 FM
Radiojamii Kilosa
0737 847 749

# Miradi ya Kimkakati Kilosa





Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akisikiliza maelezo kutoka kwa waziri wa kilimo Mhe. Hussein Bashe alipotembelea kiwanda cha kuchakata Mbegu (ASA) kilichopo Msimba Kilosa.






Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akizindua Kiwanda cha Sukari cha Mkulazi Mbigiri -Kilosa. Kiwanda hicho kina uwezo wa kuzalisha tani elfu 50 kwa mwaka .







Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akipewa maelezo wakati alipotembelea kiwanda cha kuzalisha sukari cha Mkulazi. Rais amezindua kiwanda hicho na kuwataka viongozi wa kiwanda hicho kufanya utanuzi wa kiwanda hicho.

# Mama Samia Awataka Wawekezaji Kujenga Hoteli za Kisasa Mikumi

Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Dkt. Samia Suluhu Hassan amewataka wa kuwekeza katika kujenga Hoteli za kisasa kwa wingi zitakazotumiwa na watalii watakaojitokeza nje na ndani ya nchi kufanya utalii katika Hifadhi ya Taifa ya Mikumi.

Mhe.Rais ameyasema hayo Agosti 04, 2024 wakati akizungumza na wananchi wa Mji wa Mikumi ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake wilayani Kilosa na kuongeza kuwa kupitia filamu ya Royal Tour na uwepo wa Reli ya kisasa (SGR) imeongeza watalii wengi katika Hifadhi yaTaifa ya Mikumi kutoka wageni 54,021 mwaka 2019/2020 hadi kufikia wageni 138,844 mwaka 2023/2024.

Aidha Rais Samia amesema kuwa filamu hiyo ya Utalii imekuza utalii nchini na kwa sasa serikali inawekeza kwenye miundombinu ili kurahisisha usafiri na usafirishaji wa watalii na kuwasisitizia wawekezaji kujenga hoteli za kisasa zitakazoweza kukidhi mahitaji ya watalii.

Kwa upande mwingine amesema kuwa Serikali ina lengo la kuunganisha reli iliyopo, reli yaTazara na reli ya SGR ili kurahisisha shughuli za usafiri na usafirishaji wa bidhaa na watu ili kuleta maendeleo nchini.



**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiongea na wananchi wa Mikumi wakati wa ziara yake wilayani Kilosa.**

# Sehemu ya Hotuba za Mawaziri



**Mhe. Innocent Bashungwa Waziri wa Ujenzi**

Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Samia katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ilileta hapa bilioni 45.6 kukamilisha barabara hii.

Mkoa wa Morogoro, wakati wa kipindi cha mvua za Elnino ni miongoni mwa mikoa iliyoathiriwa sana na mvua hizo.

Wizara ipo kwenye hatua za kufanya tathimini kwa ajili ya kuijenga barabara ya Dumila Mikumi kwa sababu ni muhimu kwa uchumi wa Wanakilosa na mikoa mingine kama ya Tanga na Njombe.

Tutajenga vipande vipande mpaka ikamilike na ikikamilika italeta mageuzi makubwa kwa mkoa huu na mikoa ya Kusini.

Ujenzi wa barabara pamoja na maboresho ya kiwanda cha sukari cha Kilombero umerahisishia wafanyabiashara kusafirisha bidhaa zao lakini pia miwa ya wakulima wa Ruaha na Kilombero itapata soko.

Kwakuwa kiwanda hiki kipo hapa Ruaha, na mimi nitahakikisha vijana wa hapa wanapata ajira katika ujenzi wa kiwanda hiki.

Baada ya kiwanda hiki kujengwa, ajira zaidi ya elfu nne zitapatikana na niwashauri vijana wa Ruaha mchangamkie fursa za ajira kwenye kiwanda hiki.



**Mhe. Dkt. Selemani Jafo Waziri wa Viwanda na Biashara**

Mradi mkubwa wa maji Ruaha tutahahikisha tunaukamilisha kabla ya uchaguzi wa serikali za mitaa. Na nitoe wito kwa watumishi wote wa idara ya maji kuepuka kuwabambikizia bili za maji wananchi wa Ruaha. Tumeleta maji hapa kwa wananchi wa Ruaha ili wananchi wa hapa wapate maji ya kutosha hivyo haitakuwa sawa kuwabambikia bili za maji wananchi wa hapa.



**Mhe. Jumaa Aweso Waziri wa Maji**

TAHARIRI

# Hoja Mbili Ziara ya Rais Samia Kilosa

Mhariri anazitazama hoja kuu mbili endapo zitakamilika zitainua uchumi wa kilosa na mkoa wa Morogoro kwa ujumla.
Hoja hizi ni kufuatia ziara ya siku nne ya Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan wilayani Kilosa. Hoja hizo ni;

## KUENDELEZA BONDE LA RUHEMBE

Mhe. Rais amesema kuwa serikali imetenga fedha shilingi bilioni 7.2 kwa ajili ya kuendeleza bode la Ruhembe ikiwa ni pamoja na kujenga miundombinu ya umwagiliaji na kujenga kingo za mto Ruhembe ili kupunguza athari za mafuriko.
Hii itasaidia kuinua uchumi wa wananchi wa kata za Ruaha, Ruhembe, Kidodi, Vidunda na maeneo jirani wanaotegemea bonde hilo kwa kilimo cha miwa na mpunga

## KUFUNGULIWA GATI JIPYA LA UTALII

Katika ziara ya Rais miongoni mwa hoja zilizoibuka ni pamoja na kuunganisha mtandao wa reli ya kisasa (SGR) pamoja na sekta nyingine kama utalii kwenye hifadhi ya taifa ya Mikumi.
Iwapo lango jipya la utalii litafunguliwa kupitia kata ya Kilangali, litarahisisha usafiri na usafirishaji wa wageni wanasafiri na reli ya Kisasa kutoka maeneo mbalimbali kuelekea hifadhi ya Taifa ya Mikumi.
Aidha lango hili litachochea ukuaji wa uchumi wa wakazi wa kata ya Kilangali na maeneo ya jirani lakini pia kukuza sekta ya uwekezaji.

Imechapishwa na Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

Kaimu Mkuu wa Kitengo
Elizabeth J. Makemba

Mhariri
Happiness C. Luoga

Mtengenezaji
Stamius L. Kyombo

# Je Wajua?

## Ni Kilosa Pekee Iliyotembelewa na Rais Siku nne

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amefanya ziara ya Kikazi ndani ya Wilaya ya Kilosa kuanzia tarehe 02 hadi 07 Agosti 2024.
Katika ziara yake Mhe. Rais amezindua miradi mbalimbali na kuweka majiwe ya msingi kwenye miradi kadhaa.
Aidha Rais Samia amepata nafasi ya kusalimia wananchi wa Kilosa katika maeneo ya Berega, Dumila, Kilosa mjini, Mikumi na Ruaha






# Prof. Kabudi; Mama Samia Ameleta Miradi Mingi Kilosa



*Mbunge wa Jimbo la Kilosa Mhe. Prof. Palamagamba Kabudi akiongea na wananchi wa Kilosa katika Mkutano wa hadhara kwenye ziara ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.*

Mbunge wa jimbo la Kilosa Mhe.Prof. Palamagamba Kabudi katika hotuba yake kwenye ziara ya Rais, amesema kuwa awamu ya sita imetekeleza miradi mingi ndani ya jimbo hilo katika sekta za elimu, aya na miundombinu.

Katika sekta ya elimu, mhe. Prof. Kabudi amesema kuwa zimejengwa shule mpya za sekondari, msingi na shule za kidato cha sita na tano na kuongeza kuwa miundombinu hiyo imeinua hali ya elimu ndani ya jimbo la Kilosa.

Aidha ameonza kuwa serikali imejenga vituo saba vipya vya afya huku afafanua kuwa katika sekta ya maji, imejengwa miradi mikubwa ya maji katika kata ya Dumila na Rudewa.

## Londo Aiomba Serikali Kujenga Barabara Kukuza Utalii Mikumi

Mbunge wa jimbo la Mikumi Mhe. Dennis Londo ameiomba serikali kujenga barabara ya Mikumi Kilosa kwa kiwango cha lami ili kurahisisha shughuli za utalii ikiwa ni pamoja na kusafirisha watalii wanaokuja kwa njia ya reli ya kisasa (SGR).

Ametoa kauli hiyo wakati akiongea na wananchi pamoja na wageni waliombatana na msafara wa Rais



*Mbunge wa Jimbo la Mikumi Mhe. Dennis Londo akiongea na wananchi wa Mikumi wakati wa ziara ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wilanni Kilosa*

Wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alipotembelea jimbo la Mikumi.

Aidha Mhe. Londo ameishukuru serikali ya awamu ya sita kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo Madaraja, barabara, shule za sekondari na msingi, maji, mawasiliano pamoja na vituo vya afya.

Mhe. Londo ameyataja madaraja ya Ruhembe, Mfilisi na barabara kuwa kukamilika kwake kumewasaidia wananchi wa maeneo hayo kufanya shughuli zao za kiuchumi kwa uwepesi zaidi.

# Matukio Katika Picha











